

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
**MINISTRY OF WATER**

Simu: +255 026 2322602  
Tovuti: [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)  
Barua pepe: [ps@maji.go.tz](mailto:ps@maji.go.tz)  
Unapojibu tafadhali taja:



Mji wa Serikali,  
Mtaa wa Maji,  
P. O. Box 456,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI KITAIFA (*WATER WEEK*) MWAKA 2020**

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji ilianza rasmi kuadhimisha Wiki ya Maji Kitaifa mwaka 1988 kwa kuwashirikisha Wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji. Maadhimisho hayo yanakwenda sambamba na Azimio Na. 47/193 la Umoja wa Mataifa linalozitaka nchi wanachama kuadhimisha Siku ya Maji Duniani kila mwaka ifikapo tarehe 22 Machi. Huu utamaduni wa kutambua umuhimu na thamani ya maji katika maisha ya binadamu na uchumi wa dunia kwa ujumla.

Lengo kuu la Maadhimisho ya Wiki ya Maji nchini ni kuungana na mataifa mengine duniani katika kutathimini utekelezaji, mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maji na kuainisha mikakati ya kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji nchini. Wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo hufanyika tarehe **16-22 Machi** ya kila mwaka, shughuli mbalimbali hufanyika ikiwa ni pamoja na maonesho ya teknolojia na vifaa vya maji, mikutano ya wadau na uzinduzi wa miradi.

Tofauti na Maadhimisho ya Wiki ya Maji katika kipindi cha nyuma (1988-2018), ilikubalika kwa kuanzia mwaka 2019 Mikutano yote ya mwaka ya Sekta ya Maji itafanyika wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji. Katika kipindi hiki wataalam na wadau wa maji watapata fursa ya kujadili na kubadilishana uzoefu na maarifa katika maendeleo ya Sekta ya Maji nchini. Hivyo, Maadhimisho ya Wiki ya Maji kwa mwaka 2020 yatakuwa na Kaulimbiu isemayo: **"Maji na Mabadiliko ya Tabia nchi. Uhakika wa Maji Salama kwa Wote (*Water and Climate Change: Ensuring Water Security for All*)"** na yatafanyika Jijini Dar es Salaam katika Ukumbi wa *APC Hotels and Conference*, Mbweni kuanzia tarehe **16 hadi 22 Machi, 2020**. Maadhimisho hayo yatajumuisha matukio makuu manne:

- (i) Uzinduzi wa miradi ya maji iliyokamilika
- (ii) Mkutano wa Kisayansi wa Wataalamu wa Maji (Water Scientific Conference) utafanyika tarehe **17-18 Machi 2020. Mkutano huo**

**utafunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** tarehe 17 Machi, 2020. Aidha, katika mkutano huo machapisho yafuatayo yatazinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais;

- Kitabu cha mwaka cha takwimu za haidrolojia nchini (2010-2019)
- Atlasi ya Rasilimali za Maji nchini
- Mwongozo wa Utafiti wa Maji chini ya Ardhi na Uchimbaji wa Visima

Aidha, wakati wa Mkutano huo jumla ya mada 42 zitawasilishwa chini ya maeneo yafuatayo:

- Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi,
- Njia za asili za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi,
- Usalama wa maji, nishati na chakula kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi na
- Masuala ya rasilimali fedha na uwekezaji kuhakikisha usalama wa maji nchini.

(iii) **EWURA DAY** itafanyika tarehe **19 – 20 Machi, 2020** ambayo itashirikisha Mamlaka za Maji Mijini na Wadau wengine. Mkutano huu utafunguliwa na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(iv) Mkutano wa Mapitio ya Sekta ya Maji (**Joint Water Sector Review**) ambao utafanyika tarehe **21 Machi, 2020**. Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) Waziri wa Maji atafungua mkutano. Wakati wa Mkutano matukio yafuatayo yatafanyika:

- Mapitio ya taarifa ya hali ya Sekta ya Maji kwa muda wa miaka mitano (*Water Sector Status Report 2015-2020*);
- Uwasilishaji wa *Water Sector Design Manual (4<sup>th</sup> Editions - "Highlights")*
- Uwasilishaji wa mfumo wa Sekta ya Maji wa usimamizi wa fedha (*Water Sector Portal*).

Mwisho, ninawakaribisha viongozi wote, wananchi pamoja na Wataalam wa Wizara ya Maji, Washirika wa Maendeleo, Bodi za Maji za Mabonde, Ofisi za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara na Taasisi za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Dini, Elimu ya Juu na Utafiti, Sekta Binafsi, **EWURA**, pamoja na wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji kushiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Maji kwa mwaka 2020 kwa ufanisi.

Prof. Kitila Mkumbo

**KATIBU MKUU**

12 Machi, 2020